## Tega sikio ujifunze– Elimu ya kawaida, kipindi cha kwanza.

## " Ni Vipi Plastiki hutumiwa kutengeneza mifuko?"

**Makala : Leona Frommelt**
**Tafsiri : Anne Thomas/ Eric Ponda**
**Mwelekezi: Maja Dreyer**

---

**<u>Taarifa kwa mwelekezi</u>**

**Wahusika:**
Mtangazaji
Jenny: Msichana wa umri wa miaka 14
Jack: Mvulana wa umri wa miaka 15
Mmiliki wa biashara ya mtandao wa internet

**Maeneo:**
Nyumbani,
Barabarani
Katika duka la biashara ya mtandao

**Sauti:**
Vyombo vya jikoni vikigongana
Mchakacho wa mifuko ya Plastiki
Hatua za miguu
Vyombo vya jikoni vikibebwa
Sauti ya magari barabarani
Sauti ya ndege
Sauti ya kompyuta/ kupiga chapa Kompyuta
Sauti za chini kwa chini kwenye biashara ya mtandao: sauti, kicheko, glasi, viti,

**<u>Mwanzo</u> (Mtangazaji)**

Hujambo na karibu katika msururu wetu wa makala tega sikio ujifunze, elimu ya kawaida. Wakati huu Jack ametambua tatizo sugu ambalo anamwelezea rafiki yake Jenney. Kila mwaka takriban mifuko nusu milioni ya plastiki hutengenezwa. mingi ya mifuko hiyo hutupwa kiholela. Watu wa Afrika kusini,kibeuzi huita mifuko hiyo ambayo huishia

vichakani, “ua la taifa”. Ndege na wanyama wengi wamefariki katika mbuga na jangwa baada ya kula au kumeza mifuko hiyo. Jenny na Jack wanajaribu kuchunguza jinsi mifuko hiyo inavyotengenezwa na jinsi tatizo hilo linavyoweza kukabiliwa.

**Scene 1 : Jenny anamtembelea Jack nyumbani. Ameomba baadhi ya vyombo vya nyumbani kwa sherehe aliyoandaa.**

***Sauti ya chini : Kugongana kwa vyombo***

**Jack:** nafikiri umepata kila kitu ulichohitaji. Vyungu viwili, sahani na vikombe nilivyo weza kupata.

**Jenny:** Asante -- kwa ukarimu wako wa kunipatia vyombo hivi kwa sherehe yangu. Lakini labda ungebakisha vingine ili usitumie mikono kunywa chai.

**Jack:** Hapana, nina glasi ninazoweza kutumia.

**Jenny:** Sawa. Ni vyema basi. Nitaenda nyumbani sasa kwa sababu nina mambo ninayotaka kufanya kabla ya kesho. Una mfuko wa plastiki ambao naweza kuweka vyombo hivi?

**Jack** *(Kwa hasira ):* Sina!

**Jenny** *(akiwa amechanganyikiwa) eti?*

**Jack:** Nimesema sina!!"

**Jenny:** *(Akijilaumu)* Sawa. Asante. Na ninahitajika kubeba vyombo hivi namna gani?

**Jack:** Kwa mfuko wowote ule ambao haukuundwa kwa plastiki. Mimi nimezisusia sizitumii kamwe.

**Jenny:** Kweli? Kwa nini?

**Jack:** Kwa sababu ya mazingira. Na wewe unahitajika kufanya hivyo. ukome kutumia mifuko ya plastiki.. Hujui kwamba nchi nyingi zinakataa matumizi ya mifuko hiyo.? Kwa mfano mataifa ya Afrika mashariki kama vile Kenya, Tanzania, Rwanda na Uganda wameongeza ushuru kwa mifuko hiyo na hata kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko myembamba.

**Jenny:** Aa, Sina habari kabisa!. Nina wazo Jack. Ikiwa ni muhimu kwako niache kutumia plastiki basi nisaidie kubeba vyombo hivi halafu uniambie kwa nini plastiki ni mbaya kwa maziingira. Nami nitageuza nia yangu kuhusu mifuko hiyo.

**Jack** *(Akijaribu kutafuta kisingizio):* Um, naam aaa, wajua nilifkuwa nafikiria kufanyaa……..

**Jenny:** Ulikuwa unafikiria kufanya nini?

**Jack:** *(kwa haraka)* Nilikuwa nafikiria kama naweza kukusaidia kubeba vyombo hivi.

**Jenny:** Bila shaka! …..Basi twende… *(hatua za miguu wakitoka…)*

**Muziki.....**

**Scene 2: Jenny na Jack wakiwa njiani kwenda nyumbani kwa Jenny**

***Sauti za chini kwa chini: hatua za miguu, sauti ya vyombo vikibebwa, sauti ya magari na sauti za ndege.***

**Jenny:** Sasa. Profesa sasa unaweza kuanza somo lako kuhusu mifuko ya plastiki.

**Jack:** Mifuko ya plastiki inaweza kudhuru watu na wanyama ambao hunyongwa na mifuko hiyo. Mbona huelewi? Mifuko inajaa kandokando ya barabara? Angalia kuna ule mmoja na huu ni mwingine kwenye tawi hili la mti *(akichakarisha mfuko)*. Nina hakika tutaona mingi kabla ya kufika kwenu.

**Jenny:** Ni kweli si mizuri. Haitoi sura nzuri hasa inapopeperushwa kila mahali. Na ukiangalia vizuri utaona iko kila mahali. Na ni mingi kweli.

Inakufanya kuona jinsi ambavyo tumeizoea mifuko hii.

**Jack:** Kabisa!. Ushawahi kufikiria kwa nini kuna mifuko mingi hivi kila mahali?

**Jenny:** Bado. Sina habari. Au ni kwa sababu watu wanaitumia kwa wingi na kisha kuitupa ovyo?.

**Jack:** Kabisa!. Mifuko hii ya plastiki inatumiwa mara moja na kisha kutupwa,tofauti kabisa na vikapu au mifuko ambayo inaweza kutumika mara nyingi.

**Jenny:** Na ni kwa nini mifuko hii iko kila mahali? Ni kwanini haiwezi kutupwa katika jaa la takataka?

**Jack:** Kwa kiwango fulani huwa inatupwa, lakini upepo unaipeperusha hurudishwa tena. Ukitupa kipande cha tunda kitaozea pale pale. Lakini mifuko hii haiozi, haiendi popote!.

**Jenny:** Unamaanisha nini?

**Jack:** Namaanisha kuwa mfuko mmoja unaweza kukaa miaka mingi hata miaka mia moja bila kuoza tofauti na mimea au makaratasi ambayo huchukua muda mfupi kuoza. Uchafu wa plastiki

pia hufunga mitaro ya maji machafu na ndio sababu kuna mafuriko.

**Jenny:** Bwana wee, Sijawahi fikiria kuhusu hili. Na ni kwa nini chupa na mifuko ya plastiki haiozi?

**Jack:** Bwna maswali unayouliza!Ni kwa sababu ya malighafi inayotumiwa!. Mifuko hiyo inatengenezwa na binadamu.

**Jenny:** Unamaanisha nini ukisema inatengenezwa na binadamu?

**Jack:** Yaani, binadamu ndio waliovumbua kemikali za kuunda bidhaa za plastiki. Mbao, chuma na mawe ni vitu asilia yaani vilikuwepo hata kabla binadamu kuja duniani.

**Jenny:** Kwa hivyo plastiki imeundwa na binadamu?

**Jack:** Si ndio na kuna kila aina ya plastki, ngumu kama ile inayotengeza simu, vikombe au hata fremu za miwani. Mingine ni dhaifu na inawezesha kutenegeza vitu vyembamba kama vile mifuko ya kupakia bidhaa.

**Jenny:** Na huwaje plastiki kuishia kuwa mifuko?

**Jack:** Sijui kwa sasa.. Sijui vile inavyotengezwa lakini tunaweza kwenda kwenye mtandao tufanye utafiti.

**Jenny:** Sawa!. Pia itanipa wakati wa kupumzika. Nimechoka kubeba mzigo huu wote…..

**Muziki**

**SCEN 3. Onyesho: Jenny na Jack wamekaa kwenye duka la mtandao wanafanya uchunguzi**

***Sauti za chini kwa chini,, viti, sauti za kompyutta (kupiga chapa na kipanya, inaisha chini kwa chini)***

**Jenny:** Hamjambo, kuna mashini yoyote isiyotumiwa?

**Mwenye biashara:** Angalia kule nyuma pembeni.

**Jack:** Ah, kweli kule nyuma...

**Jenny:** Sawa wacha tutafute. Mtandao unasema nini kuhusu utengezeaji wa mifuko ya plastiki?

*Jenny anapiga chapa …anatafuta*

**Jack** *(akisoma pole pole lakini kwa kueleweka):* Aha, Kuna kitu hapa chini ya kichwa "kutoka kwa Petroli hadi kwa mifuko ya plastiki". Nitaisoma. "Kiungo muhimu cha kutengeneza mifuko ya kubebea bidhaa ya po-ly-thene ni petroli. Petroli huchomwa na kutoa gesi aina ya ethene ambayo baadaye hubadilishwa kuwa plastini laini yaani *polyethylene*, ambayo ni kama uji uji. Baadaye husukumwa kwenye vishimo ambapo huunda kamba ambazo hukatwa viungo vidogo. Baadaye huchomwa, kuvutwa na kupoeshwa kuunda mifuko. Mtambo unaweza kuunda mifuko 30,000 kwa kila saa."

**Jenny:** Umeelewa?

**Jack**: Naam Kiasi!. Unahitaji pteroli ili kuunda mifuko ya platiki!. Nielewa sasa!.

**Jenny:** Ndio, na petroli ni ghali na haipatikani kwa urahisi. Ikiisha imekwisha kabisa!. Kwa hivyo ni kupoteza rasilmali kuunda mifuko mingi ya plastiki na petroli. Hata sijui ni mifuko mingapi ambayo imeundwa duniani kote.

**Jack:** Inasema hapa kuwa kila mwaka mifuko bilioni mia 6 huundwa.

**Jenny:** Lakini huo ni upuzi! . Sasa nini faida ya mifuko hiyo kwa sababu haiozi na haitumiwi tena?

**Jack:** Wacha tuone mtandao wa internet unasema nini kuhusu kutupa mifuko ya plastiki.

*Jenny anapiga chapa …anatafuta*

**Jenny** *(Anatafuta na kusoma kwa sauti kubwa):* hapa kuna maneno kuhusu uchafu wa plastiki. “Er, blah.. di…blah.. di blah, majiko ghali ya kuchoma taka si suluhisho. Plastiki inapochomwa inatoa gesi yenye sumu aina ya Chlorine, ambayo, kwa mfano inachafua mazingira na kuchangia kuongezeka kwa joto ulimwenguni. Pia kuna madini yenye sumu yanayobaki ardhini. Kadhalika si rahisi kuchoma taka aina ya plastiki kwa sababu ina bidhaa nyingine. Bidhaa za plastiki haziwezi kuchomwa pamoja na takataka za plastiki,zinapongoja kuchomwa huwa zinaongezeka na kufanya rundo, na hata wakati mwingine kuchafua maji.

**Jenny** *(Kwa hasira ):* inasikitisha!

**Jack**: tumejifunza nini sasa

**Jenny**: Ni lazima tupunguze matumizi ya bidhaa za plastiki!. Na kitu cha kwanza ni kuhakikisha tunaacha kutumia mifuko ya plastiki. Ngoja kidogo. Nataka kwenda sasa!

***Sauti ya chini kwa chini ( Jenny anataka kwenda)***

**Jack:** Ala ni nini wewe? Mbona unaenda haraka hivyo?

**Jenny:** Kwani hauelewi? Naenda kuanzisha kampeini dhidi ya mifuko ya plastiki. Kwanza lazima niwaeleze wote wanaokuja kwa sherehe yangu wasije na mifuko ya plastiki. Wote! bila kubagua!.

**Jack:** Inamaanisha nimekuelimisha vya kutosha kuhusu ubaya wa mifuko ya plastiki.

**Jenny:** Kweli kabisa!. Jack njoo. Hatuna wakati wa kupoteza. Ni lazima uweke vinywaji katika chupa. Chupa za glasi lakini.

**Jack:** Hapana…

**Muziki**

**<u>Mwisho</u> (Mtangazaji)**

Labda sasa Jack ataanza kubeba chupa za glasi kwenye vikapu. Baada ya sherehe,m utafiti zaidi utaendelea kujifunza mengi zaidi. Jack na Jenney hawachoki kutafuta majibu kwa maswali yanayokuwa nayo kichwa. Ni hayo tu kwa leo kutoka kwa vipindi vyetu “tega sikio ujifunze” “elimu ya kawaida” vinavyotayarishwa na Leona Frommelt. Pia unaweza kutusikiliza kupitia mtandao wetu www.dw.de/kiswahili. Asante na usisahau kututegea wakati mwingine